**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

# MWONGOZO WA MAZISHI SALAMA NA YENYE UTU KWA MTU ALIYETHIBITIKA AU KUHISIWA KUFARIKI KWA COVID-19

## Toleo la Kwanza Tarehe 26 Mei, 2020

Mlipuko wa Ugonjwa wa homa kali ya mapafu (COVID-19), ambao umezikumba nchi zote duniani, umeathiri mikoa kadhaa hapa nchini. Kulingana na kanuni za kudhibiti maambukizi wakati wa milipuko, na kwa mujibu wa Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009, inaelekeza taratibu za kufuata wakati wa mazishi ikiwa ni pamoja na mazishi ya maiti husika kufanywa chini ya usimamizi wa mamlaka za Kiserikali ambazo zitazingatia usalama na kuzuia maambukizi kwa jamii kama ilivyoelekezwa hapa chini.

1. **Mambo ya Kuzingatia endapo Mgonjwa au Mshukiwa wa COVID 19 anapofariki**
   a. Mazishi yafanyike kwa utu na heshima ya binadamu
   b. Familia ishirikishwe kikamilifu katika taratibu za mazishi, pamoja na mahala pa kuzikwa
   c. Inashauriwa kwa kadri itakavyowezekana, maiti izikwe ndani ya muda usiozidi masaa 48 baada ya kukabidhiwa ndugu /familia. Hairuhusiwi kabisa kuufungua mwili ukishaandaliwa na kuhifadhiwa na wataalamu kwenye sanduku maalumu la mazishi.
   d. Familia inaweza kusafirisha maiti kwa kuzingatia maelekezo na uangalizi maalumu wa Afisa wa Afya, mpaka sehemu ya kuzika
   e. Kama marehemu alikuwa mhisiwa (suspect) vipimo vya maabara vichukiliwe haraka ndani ya masaa 3 na kuruhusu familia kuendelea na mazishi. Aidha, kusubiri majibu isiwe sababu ya kuzuia maiti kuzikwa au kusafirishwa huku kanuni zote za kudhibiti maambukizi zikizingatiwa hivyo tahadhari zote zichukuliwe wakati wa kuzika sawa na mtu aliyethibitika kufariki kwa COVID-19.

f. Washiriki wa mazishi wanatakiwa kuepuka misomgamano na kukaa umbali wa zaidi ya mita moja kutoka mtu mmoja hadi mtu mwingine.
g. Taratibu za ibada, zinaruhusiwa kufanyika katika eneo la mazishi, Kiongozi wa Dini asimame umbali wa takribani mita 2 kutoka eneo maiti/jeneza ilipolazwa na ataruhusiwa kutumia muda usiozidi saa moja.

h. Mazishi wakati wa mlipuko yatasimamiwa na maafisa wa serikali walioteuliwa kwa kushirikiana na ndugu.

**2. Timu ya Wataalamu wa mazishi**

a. Timu ya Wazikaji waliopata mafunzo walau wanne (4) au zaidi.
b. Mtaalamu wa Afya atakayesimamia Mazishi (Awe Mtaalamu wa Afya Mazingira).
c. Kiongozi wa Kiimani.
d. Afisa ustawi wa jamii, kuwezesha mawasiliano sahihi kati ya Wanafamilia na Timu ya Wazikaji.
e. Mtaalamu wa Kuzuia na kudhibiti maambukizo (Infection Prevention and Control). (Ambaye atahakikisha wahusika wote wanafuata taratibu za kuzuia maambukizi wakati wa mazishi).

**3. Vifaa kwa ajili ya Mazishi**

a. Mfuko maalumu kwa ajili ya kuhifadhia maiti (burial body bag)-
b. Mavazi kinga kwa ajili yaTimu ya Mazishi.
c. Dawa ya kuambukua (Kiambukuzi -Disinfectant mfano chlorine).
d. Kifaa Maalumu cha kuchanganyia na kuhifadhia kiambukuzi.
e. Jeneza kwa kadri Imani ya marehemu itakavyoelekeza.

**4. Taratibu za kusafirisha**

a. Inashauriwa mwili wa marehemu kuzikwa ndani ya Halmashauri ambapo mgonjwa au mshukiwa wa COVID 19 amefariki
b. Endapo kuna ulazima wa kusafirisha mwili itakuwa ni lazima mwili ufungwe kwenye mfuko maalumu wa kuzikia (burial bag) ambao ni imara na kuwekwa ndani ya sanduku imara kuepuka kuvuja au kupasuka.
c. Ndugu wasiozidi wawili tu wa familia ya marehemu ndio watakaoruhusiwa kusafiri na mwili kwenye gari au chombo chochote cha usafiri ambapo ni lazima wapewe elimu ya kusafiri na mwili bila kuufungua na kutoa taarifa kwa Afisa afya kama kutakuwa na shida ya bag kuvuja au kupasuka.

d. Gari itakayobeba mwili wa marehemu ifanyiwe usibuaji mara baadaya kushusha mwili wa marehemu.
e. Mawasiliano ya awali yafanyike na Afisa afya katika halmashauri ambapo marehemu atazikwa ili kuhakikisha taratibu za usalama zimezingatiwa.

**5. Taratibu za Mazishi**

a. Mwili wa marehemu utaandaliwa na Timu ya Wazikaji kwa kufuata taratibu za kuzuia maambukizi ikiwa ni pamoja na kuvaa vifaa Kinga, na kisha kuwekwa ndani ya Jeneza na kufanya usibuaji (Decontamination)
b. Ndugu wanaweza kukabidhiwa mwili kwa ajili ya kuendelea na taratibu za Mazishi huku wakizingatia kanuni za kudhibiti maambukizi kwa usimamizi wa Afisa wa Afya Mazingira.
c. Kabla ya kuelekea makaburini, Mtaalamu wa Afya (avae vifaa kinga, mask, face shield/goggles na apron), anaweza kufungua sehemu ya juu (uso) ya Mfuko maalumu wa Mazishi kwa ajili ya kuruhusu ndugu kuweza kuona Mwili wa mpendwa wao bila kugusa wakiwa wamevaa vifaa kinga.
d. Watakaohusika na mazishi wanatakiwa kuvaa vifaa kinga muhimu tu (Barakoa, Miwani, GlavungumunaApron (surgical Mask, Goggles/Face shield, Heavy duty apron&utilityGloves).
e. Taratibu za ibada, zinaruhusiwa kufanyika katika eneo la mazishi, Kiongozi wa Dini asimame umbali wa takribani mita 2 kutoka eneo maiti/jeneza ilipolazwa
f. Baada ya Mazishi, washiriki wa mazishi wote, watatakiwa kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni kabla ya kuondoka eneo la makaburi.
g. Gari iliyobeba mwili wa marehemu itafanyiwa usibuaji (decontamination) kabla ya kuondoka eneo la makaburi kwa kuzingatia miongozo ya usibuaji chini ya usimamizi wa Mtaalamu wa Afya.
h. Ndugu wafahamishwe kuwa hawaruhusiwi kufanya matanga ili kuepuka mikusanyiko ya watu

**6. Wajibu wa ndugu wa Marehemu.**

a. Kuandaa eneo la mazishi na kuchimba kaburi (Makaburi ya jumuiya yanapendekezwa zaidi).
b. Ndugu wa marehemu watahakikisha kunakuwepo na sehemu maalumu ya kunawa mikono katika eneo la makaburi (Maji tiririka na sabuni).

**7. Wajibu wa Mamlaka ya eneo ambapo marehemu anazikwa**

a. Mamlaka ya eneo husika, ihakikishe inatoa Msimamizi wa mazishi (Awe Mtaalamu wa Afya Mazingira) kuhakikisha afua za kuzuia maambukizi zinazingatiwa wakati wa mazishi.
b. Msimamizi wa mazishi ataratibu shughuli nzima ya mazishi kwa kushirikisha ndugu wa marehemu.

Utaratibu huu utaendelea kufuatwa mpaka hapo Wizara itakapotoa utaratibu mwingine.

Prof. Abel N. Makubi
**MGANGA MKUU WA SERIKALI**